HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE | TOLEO LA 008 | SEPTEMBA 2024 | HALIUZWI

Jarida la

# TEMEKE YETU

FAHAMU ZAIDI



## "HAMASISHENI VIJANA NA WANAWAKE WASHIRIKI KUIJENGA TANZANIA YETU

HABARI KAMILI UK. 03

NDANI



## NAIBU KATIBU MKUU AFURAHISHWA NA KASI YA UJENZI WA HOSPITALI MBAGALA

Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tamisemi anayeshughulika na Afya Dkt Charles Mahera amefurahishwa na kasi ya ujenzi wa jengo la ghorofa sita la hospitali ya Mbagala Rangitatu...

**MHARIRI MKUU**

**JOANITA JOSEPH**

**KAIMU MKUU - KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**

**MANISPAA YA TEMEKE**

**WAHARIRI WASAIDIZI**

**MUSSA CHISONGELA**

**SWEETBETTER NJIGE**

**REHEMA ISANGO**

**MSANIFU WA JARIDA**

**SIMON JOSHUA**

**WAPIGA PICHA**

**GERVAS EDICK**

**SHAMSI MUSTAPHA**

**JARIDA HILI HUTOLEWA NA KITENGO CHA HABARI**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE**

**S.L.P 46343 TEMEKE, DSM.**

**SIMU: +255 22-2928132**

**NUKUSHI: +255 22-2928137**

**BARUA PEPE: TEMEKE@TEMEKEMC.GO.TZ**

**TOVUTI: WWW.TEMEKEMC.GO.TZ**



# HAMASISHENI VIJANA NA WANAWAKE WASHIRIKI KUIJENGA TANZANIA YETU

Na Sweetbetter Njige,
TMC Habari.

Kuelekea uchaguzi wa Serikali za mitaa utakaofanyika Novemba 27, 2024 mkuu wa mkoa wa Dar es salaam Albert Chalamila ametoa wito kwa wakazi wa wilaya ya Temeke kushiriki uchaguzi kwa kujiandikisha, kuchagua pamoja na kugombea nafasi za Uongozi. .

Akizungumza na Wananchi katika kituo cha afya Kilakala (Kilichopandishwa hadhi hivi karibuni) mhe. Chalamila amesema baadhi ya Wananchi hawashiriki uchaguzi badala yake hutoa lawama juu ya uongozi bila kuchukua hatua.

"Muda umekaribia, zoezi la kujiandikisha likifika twende tukajiandikishe, vijana na wanawake nawasihi tujitokeze kugombea hizi nafasi kwasababu miongoni mwetu wapo watu ambao kazi yao ni kulaumu, yule mwenyekiti mwizi, yule mjumbe hafanyi kazi yake ukiuliza si ulimchagua anasema hapana, uligombea hapana. Hamasisheni vijana wanaoweza washiriki kuijenga Tanzania yetu. Shiriki kwa kujiandikisha ili tuwe na matunda mazuri kiasiasa na kiuchumi".

Aidha mhe. Chalamila ametoa wito kwa wazazi kuzingatia malezi bora kwa watoto hususani ili kuondoa tabia na mlipuko wa matukio yasiyofaa katika jamii.

"Leeni watoto wenu vizuri, hasa kwa wale wazawa. Wafunzeni vijana wenu kuwa na nidhamu. Mtu anaenda kuiba mali ina thamani ya shilingi milioni 100 anasahau thamani ya maisha yake ni kubwa kuliko hicho anachoiba. Wengine wanashiriki katika matukio maovu ikiwemo utekaji mifano ipo na mnaijua lakini lawama wanabebeshwa Polisi.

Kama tunataka kujenga Taifa letu likiwa salama na imara lazima tuulizane na kujibu maswali ya msingi".

Mhe. Chalamila amefanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo katika wilayani Temeke na kukagua miradi hiyo ya maendeleo ikiwemo ujenzi wa bweni na bwalo shule ya sekondari Kibasila, kituo cha afya Kilakala, zahanati mpya ya kurasini na ujenzi wa ofisi ya kata ya Miburani.

UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA
JIANDIKISHE PIGA KURA
2024
OFISI YA RAIS TAMISEMI

# MTINIKA AKABIDHI 'SITE' KWA MKANDARASI, UJENZI HOSPITALI YA WILAYA KUANZA

Na Shalua Mpanda,
TMC Habari.



Mstahiki meya wa manispaa ya Temeke mheshimiwa Abdallah Mtinika leo Agosti 31,2024 amemkabidhi rasmi mkandarasi kampuni ya Mnico Construction eneo la Vikuruti Chamazi ambapo panatarajiwa kujengwa hospitali ya Wilaya Temeke.

Meya Mtinika amekabidhi eneo hilo ikiwa ni baada ya muda mrefu wa wananchi kusubiri kwa hamu ujenzi wa hospitali hiyo inayotarajiwa kuwa suluhisho la huduma za afya Temeke.

Amemtaka Mkandarasi huyo kufanya kazi kwa muda uliopangwa ili wananchi wapate huduma za afya katika eneo Wilaya hii na maeneo ya jirani ikiwemo wilaya ya Mkuranga.


"Mimi napenda sana spidi hivyo nitafurahi sana kazi hii ikimalizika kwa wakati".Alisema Mtinika

Mkurugenzi wa kampuni hiyo iliyokabidhiwa eneo hilo ndugu Werema Mnico amesema ujenzi wa jengo la kwanza la Wagonjwa wa Nje(OPD) unatarajiwa kuanza siku ya Jumanne wiki ijayo.

Ujenzi wa Hospitali hiyo ni utekelezaji wa Sera ya Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mhe.Dkt.Samia Suluhu Hassan ya kuboresha huduma za Afya hapa nchini.

SOMA MATOLEO MENGINE YA JARIDA LA TEMEKE YETU KUPITIA TOVUTI YA TEMEKEMC.GO.TZ






# HOSPITALI YA RUFAA TEMEKE KUTOA HUDUMA ZA TIBA YA FIGO NA KUOKOA UHAI WA MAMA NA MTOTO

Na Joanita Joseph,
TMC Habari.

Mkuu wa Wilaya ya Temeke Mhe. Sixtus Mapunda leo Agosti 12, 2024 amemuwakilisha Waziri wa Afya Mhe. Ummy Mwalimu (Mb) katika hafla ya Uzinduzi wa Jengo la kutolea huduma za usafishaji Damu kwa Wagonjwa wa figo (Dialysis) sambamba na Uzinduzi wa gari la Wagonjwa wa dharura maalum kwa ajili ya Mama na Mtoto ili kuwezesha upatikanaji wa huduma kwa haraka na usalama.

Jengo hilo ni moja ya maboresho katika Hospitali hiyo kwa Ufadhili wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA) iliyochangia zaidi ya Milioni 200 limelenga kutoa huduma nafuu ya kusafisha damu na kusaidia kupunguza mrundikano wa wagonjwa wanaohitaji huduma hoyo katika Hospitali ya Taifa Muhimbili.

Akizungumza katika Hafla hiyo DC Mapunda amewataka Wananchi kuzingatia Afya zao na kufata mtindo bora wa Maisha ili kuepuka Magonjwa yasio ya kuambukiza ikiwemo kisukari, presha na matatizo ya figo.

“Kwa kipindi cha miaka mitatu ya Serikali ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Serikali imefanya mapinduzi makubwa katika Sekta ya Afya na ni mpango wa Serikali kuhakikisha huduma za Afya zinasogezwa karibu na Wananchi. Lakini pamoja na hayo nasisitiza jamii kufata mtindo bora wa maisha ili kuepuka magonjwa yasiyo ya kuambukiza ambayo yamekuwa yakiongezeka kwa kasi” alisema DC Mapunda



Nae Daktari Joseph Kimaro, Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo amesema Temeke imekuwa ikipokea Wagonjwa wengi wanaohitaji huduma hivyo.

# SATURA AKABIDHIWA RASMI MANISPAA YA TEMEKE

Na Sweetbetter Njige,
TMC Habari.

Leo Agosti 19,2024 Mstahiki Meya wa Manispaa ya Temeke Mheshimiwa Abdallah Mtinika ameongoza makabidhiano ya Ofisi baina ya aliyekuwa Mkurugenzi wa Manispaa yaTemeke Ndg. Elihuruma Mabelya na Mkurugenzi mpya Ndg. Jomary Mrisho Satura mbele ya watumishi wa manispaa kufuatia Uhamisho wa Wakurugenzi Watendaji wa Halmashauri uliofanywa na Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan mnamo Agosti 14, 2024.

Akizungumza katika makabidhiano hayo Mhe. Mtinika amewataka watumishi kuhakisha wanafungua ukurasa mpya na kujituma kutokana na maelekezo ya uongozi mpya.

"Tumepata kiongozi mpya itatubidi sisi wenyewe kama watumishi kuwa 'flexible', tunafurahia mabadiliko haya aliyoyafanya Mhe. Rais na kwakuwa ameyafanya yeye tunaamini yana nia njema. Satura karibu sana Temeke, karibu kwa uhuru kabisa na falsafa zako, njoo na falsafa zako usiogope ku 'apply' kwa sababu ilikuwa hivi basi nisi apply falsafa hizi, na sisi tunakuahidi kila aina ya sapoti kutoka kwetu utaipata, tutakuunga mkono kwa 100% Tuiweke Temeke mbele tufanye kazi kwa maslahi ya Wananchi wa Temeke".

Nae Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke Ndg. Jomary Satura amesema yupo tayari kutekeleza malengo makuu ya Serikali kama mtumishi kiongozi
"Jukumu kubwa la Serikali ni utawala na kuwaletea Wananchi maendeleo lakini wajibu wetu kama Viongozi na watumishi ni kukidhi matarajio ya jamii. Naamini, msingi wa yote hayo majukumu mawili ni utayari ikiwa ni pamoja na kukataa kushindwa. Sina kitu chochote zaidi yenu kama timu ya ushindi"

Aidha Mkurugenzi wa Jiji la Dar es salaam Ndg. Elihuruma Mabelya ametoa shukrani zake kwa Baraza la Madiwani, Watumishi, na Wananchi wote wa Temeke kwa kipindi chote alichohudumu kama Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke.



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE**

**Tarehe:** 10/07/2024

# TANGAZO

MKURUGENZI WA MANISPAA YA TEMEKE ANAWATANGAZIA WAMILIKI WOTE WA MAJENGO YA BIASHARA, VIWANDA, MAGHOROFA, MAKAMPUNI, MAKAZI, TAASISI ZISIZO ZA KISERIKALI NA MAJENGO YOTE AMBAYO HAYALIPI KODI KUPITIA MFUMO WA MITA ZA LUKU, KUFIKA KATIKA OFISI ZA MANISPAA YA TEMEKE ILI KUSAJILIWA KWENYE MFUMO NA KUPATIWA NAMBA ZA MALIPO ILI WAWEZE KULIPA KODI YA MAJENGO INAYOTAKIWA KULIPWA KILA MWAKA.

WALE WOTE WENYE MSAMAHA WA KODI WANAPASWA KUFIKA OFISI ZA MANISPAA NA MUHTASARI KUTOKA OFISI YA KATA KAMA UTHIBITISHO WA KUSAMEHEWA KODI HIYO.

NA KWA WALE WANAONDELEA KULIPA KODI ZA MAJENGO WANAPASWA KUFIKA KATIKA OFISI ZA MANISPAA NA KITAMBULISHO/NAMBA YA NIDA, NA NAMBA ZA SIMU ZINAZOPATIKANA.

KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA SIMU AU TUMA UJUMBE MFUPI WA MANENO (SMS/WHATSAPP) KWA NAMBA 0766 275 123 KWA MSAADA ZAIDI.

KUMBUKA KUTOKULIPA KODI YA JENGO NDANI YA MUDA ULIOWEKWA KISHERIA KUTASABABISHA MMILIKI WA JENGO KUVUNJA MOJA YA SHARTI LA UMILIKI HIVYO HATUA ZA KISHERIA ZITACHUKULIWA DHIDI YAKE.

**TANGAZO LIMETOLEWA NA;**

Joanita J. Ntamuti

**KAIMU MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI**
**MANISPAA YA TEMEKE**



# MENEJIMENTI YAHITIMISHA ZIARA YENYE MAFANIKIO

Na Sweetbetter Njige,
TMC Habari.

Jumla ya miradi 9 imetembelewa na kukaguliwa na Menejimenti ya manispaa ya Temeke kupitia ziara ya siku mbili (Agosti 14 na 15, 2024) kwa kutembelea na kukagua jumla ya miradi 9 ya maendeleo inayotekelezwa katika kata mbalimbali ndani ya manispaa ya Temeke.

Akizungumza katika majumuisho kiongozi wa ziara hiyo na mkuu wa idara ya Maendeleo ya Jamii bi. Furaha Chiwile amesema ziara hiyo imekuwa na mafanikio makubwa kutokana na uhalisia wa utendaji kazi unaoridhisha kutoka kwa wataalam na wasimamizi waliokabidhiwa miradi hiyo kwa kuzingatia kasi inayoendana na thamani ya fedha.

Aidha Bi. Chiwile amesema menejimenti imepokea changamoto, maoni, mapendekezo yaliyotokana na ziara hiyo na ipo tayari kuziwasilisha kwa mkurugenzi wa Manispaa ili zifanyiwe kazi kwa wakati kwa manufaa ya wakazi wa Temeke.

Miradi iliyotembelewa ni pamoja na upanuzi wa hospitali ya Mbagala rangitatu (Ghorofa sita) mradi unaogharimu shilingi bilioni 10.8 ambao ujenzi wake umefikia 60%, shule mpya ya sekondari Maganya (kata ya Mbagala) yenye ghorofa tatu, vyumba vya madarasa 16, matundu ya vyoo 40, ofisi 8 na miundombinu ya watu wenye ulemavu,ujenzi wa ukuta wenye urefu wa futi 2.5 kwenda juu na mita 420 kuzunguka eneo la shule ya msingi Kilamba,uwezeshaji wa vifaa tiba kituo cha afya Mkondogwa kata ya Chamazi, ukamilishaji wa jengo la utawala shule ya msingi Tandika, bweni la wavulana shule ya sekondari Mikwambe, ujenzi wa bweni la wavulana shule ya sekondari Mikwambe na mingineyo.

## Fikra za Satura



**“Serikali ina Majukumu makubwa mawili, Jukumu la kwanza ni Utawala na la pili ni kuwaletea Wananchi Maendeleo. Wajibu wetu Sisi Viongozi ni kukidhi matarajio ya Wananchi kwa Serikali yao....sasa hapa kwenye matarajio ndipo kama Kiongozi unaangalia timu uliyonayo, Je inakidhi matarajio? Ninaamini ninyi ni timu ya Ushindi, Tufanye kazi!”.**

**- Jomaary Mrisho Satura**
**Mkurugenzi Manispaa ya Temeke**



*Hospitali ya Mbagala Rangitatu itakayogharimu Tsh. 10.8 Bilioni hadi kukamilika kwake, ilianza kujengwa mwaka 2018/2019 huku ikitarajiwa kukamilika Agosti 2025 na itasaidia wagonjwa mbalimbali ndani na nje ya Dar es Salaam.*

# SERIKALI YAFURAHISHWA NA UJENZI HOSPITALI MBAGALA

Na Shalua Mpanda,
TMC Habari.

Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tamisemi anayeshughulika na Afya Dkt Charles Mahera amefurahishwa na kasi ya ujenzi wa jengo la ghorofa sita la hospitali ya Mbagala Rangitatu.

Akizungumza na watendaji wa Halmashauri ya manispaa hiyo katika ziara yake aliyoifanya leo Julai 2,2024 katika eneo hilo amesema hapo awali ujenzi huo ulikuwa unasuasua kuanza kutokana na baadhi ya mambo kutokukamilika lakini ameshangaa kuona ujenzi huo umefikia asilimia karibu 50.

“Leo sina mengi zaidi ya kuwapongeza kwa yale tuliyokubaliana hapa mmetekeleza kwa kasi ya ajabu”.Alisema Katibu huyo.

Kwa upande wake Meya wa manispaa ya Temeke mheshimiwa Abdallah Mtinika amemshukuru Naibu Katibu mkuu huyo kwa kuwa mstari wa mbele kufuatilia ujenzi huo mara kwa mara na kumuahidi kuwa atahakikisha wanasimamia ujenzi huo uishe kwa wakati.

Mkurugenzi wa manispaa ya Temeke ndugu Elihuruma Mabelya amesema ujenzi huo ambao mpaka kukamilika kwake utatumia Shilingi bilioni 10.8 ni juhudi za Mhe.Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kuhakikisha anaboresha huduma za Afya kwa wananchi.

Jengo hilo litakapokamilika litasaidia kupunguza msongamano wa wagonjwa katika Hospitali hiyo ambayo kwa sasa inahudumia wagonjwa zaidi ya elfu moja kwa siku.

# MRADI WA DMDP AWAMU YA PILI MBIONI TEMEKE

Na Joanita Joseph,
TMC Habari.

Ni maandalizi ya Mradi wa Dar es salaam Metropolitan Development Project (DMDP) Awamu ya pili ambapo leo Julai 17, 2024 wakandarasi wametembelea miundombinu inayotarajiwa kuendelezwa ikiwemo barabara na vivuko kupitia Mradi huo ili waweze kujaza zabuni zilizotangazwa kwa ajili na na timu hiyo kujionea mikakati pamoja na kutoa maelekezo kadhaa kwa Manufaa ya Wananchi wa Jimbo la Temeke.

Akizungumza akiwa katika barabara ya Pendamoyo, Temeke Mhe. Kilave amesema

"Uboreshaji wa barabara na vivuko utaimarisha uchumi kwa wanaTemeke lakini hata athari za mafuriko pia zitapungua kwa kiasi kikubwa, mradi huu utakMasuliza, kilimahewa, konisaga, kurasini, taningira, uhasibu, pendamoyo, pendamoyo 1, kizota, Mandera, lushoto, mkumba, pamoja kivuko cha shehe Mucki, Baajun, Mpeta na Mdeda.

Ikumbukwe kuwa mnamo Februari 21, 2024 Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Benki ya Dunia zilisaini Mkataba wenye thamani ya Euro 361.1 sawa na Bilioni 988.083 kwa ajili ya kuboresha Miundombinu muhimu ya umma na huduma jijini Dar es Salaam ikiwemo wilayani Temeke ambapo takribani barabara zenye jumla ya kilomita 52.71 zinatarajiwa kuboreshwa kwa kiwango cha lami/zege pamoja na ujenzi wa vivuko 8 wilayani Temeke.

Ujio wa Mradi huu (DMDP Phase 2) utakwenda kubadilisha tas-



ya kuwapata wakandarasi watakaotekeleza jukumu hilo.

Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Temeke Mhe. Dorothy Kilave naye alipata wasaa wa kuungawenda kuboresha maisha ya wanaTemeke, mimi niwatakie kila la kheri tukachape kazi" alisema Mhe. Kilave
Miongoni mwa barabara zilizotembelewa leo ni pamoja na

wira ya Manispaa ya Temeke na kurahisisha usafiri kwa Wananchi kutoka eneo moja kwenda jingine jambo litakaloongeza chachu katika ukuaji wa vipato vyao na pato la Taifa kwa ujumla.

# MENEJIMENTI YA MANISPAA TEMEKE YATEMBELEA MAONESHO YA NANENANE MOROGORO

Na Shalua Mpanda,
TMC Habari.

Leo ikiwa ni siku ya saba toka kuanza kwa Maonesho ya Nanenane katika viwanja vya Mwalimu Nyerere mkoani Morogoro, baadhi ya Wakuu wa Idara na Vitengo kutoka Manispaa ya Temeke wametembelea Maonesho haya.

Wakiwa katika banda la manispaa ya Temeke,viongozi hao wamejionea shughuli mbalimbali zinazofanywa na Wakulima na Wajasiriamali kutoka katika Manispaa hiyo.

Mkuu wa Idara ya Viwanda na Uwekezaji Ndg. Ramadhan Gurumukwa akiongea kwa niaba ya wakuu wa Idara wengine,amesema kumekuwa na mabadiliko makubwa katika bidhaa mbalimbali zinazozalishwa na vikundi vya wajasiriamali ukilinganisha na miaka iliyopita.

“Hongereni sana kwa ubora wa bidhaa hizi na sisi kama Serikali tutaendelea kuwaunga mkono katika kuhakikisha bidhaa zenu zinaendelea kuwa bora”.Alisema Gurumukwa.

Baadhi ya wakuu wa Idara waliotembelea banda la Manispaa hii ni pamoja na Mkuu wa Idara ya Uchumi na Mipango Ndg.Gervas Lupembe,Mkaguzi wa ndani Ndg. Henry Nyaulingo, Mkuu wa Kitengo cha Tehama Ndg. Yahya Madenge na wengineo




## MEYA MANISPAA YA TEMEKE AKABIDHI BENDERA YA TAIFA TIMU YA WATUMISHI

Na Mwandishi Wetu,
TMC Habari.

Mstahiki Meya wa Manispaa ya Temeke Mhe. Abdallah Mtinika leo Agosti 23, 2024 amekabidhi Bendera kwa Timu ya Watumishi wa Manispa hii wanaokwenda kushiriki michezo ya Shimisemita inayotarajiwa kuanza Mnamo Agosti 25, 2024 Jijini Mwanza.

SHIMISEMITA ni Shirikisho la Michezo ya Serikali za Mitaa Tanzania inayolenga kuendelea kuboresha na kuimarisha Afya za Watumishi wa Serikali za Mitaa kupitia michezo.

Jumla ya timu 66 zitashiriki mashindano hayo ya SHIMISEMITA 2024 yatakayofanyika Jijini Mwanza kuanzia tarehe 25 Agosti, 2024 na kuhitimiswa Septemba 5, 2024.

“Shimisemita 2024, Shiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa Taifa endelevu”.

# CHALAMILA AKABIDHI GARI MPYA KWA WAKUU WA WILAYA

Na Joanitha Joseph,
TMC Habari.

Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mhe. Albert Chalamila leo Septemba 30, 2024 amekabidhi gari mpya aina ya Prado TX (Zero kilometres) kwa Wakuu wa Wilaya ya Temeke na Kinondoni ikiwa ni katika kuimarisha utoaji huduma kwa Wananchi hasa katika kuwafikia lakini pia kufanya Ukaguzi wa Miradi mbalimbali ya Maendeleo.

RC Chalamila ameeleza kuwa magari hayo yametolewa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan ili kazi ziweze kufanywa kwa ufanisi na kuboresha utoaji huduma kwa Wananchi ikiwa ni pamoja na utatuzi wa migogoro kwa haraka.

"Mheshimiwa Rais ameleta fedha nyingi katika Mkoa wetu wa Dar es Salaam, hatuwezi kutembea kwa miguu kila mahali chombo hiki kikatumike kukagua Miradi ya umma, miradi ya Serikali na kusikiliza Wananchi pale ambapo wana dukuduku pale ambapo wana jambo lolote..Magari haya yatunzwe na yatumike katika shughuli za kumsaidia Mheshimiwa Rais kuwafikia Wananchi na kutatua kero" Alisema RC Chalamila

Vilevile RC Chalamila amesema kuwa magari hayo yatasaidia pia katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika Novemba 27, Mwaka huu lakini pia hata Uchaguzi Mkuu Mwakani kwa kuwawezesha Viongozi hao kufika katika maeneo mbalimbali

"Kuelekea Novemba 27, 2024 Siku ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, lazima Wakuu wa Wilaya wawe na vyombo vya kusaidia masuala yote ya Uchaguzi ili uwe huru na haki"





*Maadhimisho ya siku ya lishe kitaifa mwaka huu yatafanyika Tarehe 30 Oktoba 2024 katika viwanja vya Bustani, Kijichi, Temeke. Maadhimisho hayo yanalenga kukuza uelewa wa jamii juu ya mambo ya lishe na magonjwa yahusuyo lishe.*

# DC MAPUNDA AFURAHISHWA NA MKATABA WA LISHE TEMEKE

Na Shalua Mpanda,
TMC Habari.

Mkuu wa wilaya ya Temeke mheshimiwa Sixtus Mapunda ameonesha kufurahishwa na utekelezaji wa mkataba wa Lishe unaotekelezwa katika Manispaa hii.

Akiongea katika kikao kilichojumuisha watendaji wa kata zinazounda manispaa ya Temeke,Mhe.Mapunda amesema pamoja na kufanya vizuri katika kutekeleza Mkataba huo,mikakati zaidi inapaswa kuwekwa ili kuendelea kufanya vizuri zaidi.

"Kwa kweli Temeke tunafanya vizuri zaidi ukilinganisha na nilipotoka,na hili niliweke bayana... kama tunavyofahamu ajenda hii ni ya mheshimiwa Rais,hatuna budi kutilia mkazo suala la lishe". Alisisitiza Mkuu huyo wa Wilaya.

Kwa upande wake Mratibu wa Lishe wilaya ya Temeke Bi.Happy Nkunda akitoa ufafanuzi kwa mkuu wa Wilaya,amesema wamefanikiwa kutimiza malengo ya Mkataba huo kwa zaidi ya asilimia 90 kutokana na ushirikishwaji wa wadau wa Lishe.

*Kila Oktoba 30 ni maadhimisho ya siku ya lishe kitaifa*

Manispaa ya Temeke imekuwa mstari wa mbele kutekeleza Mkataba wa huo kwa kushirikisha Idara mbalimbali za Manispaa hii huku ikiwekeza nguvu katika kutoa elimu ya lishe bora hasa katika shule za Msingi na Sekondari.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe.Dkt. Samia Suluhu Hassan akiambatana na Rais wa Jamhuri ya Msumbiji Mhe. Filipe Jacinto Nyusi ambaye ni Mgeni Rasmi katika sherehe za ufunguzi wa maonesho ya 48 ya biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam, wakipita katika mabanda mbalimbali leo Julai 03, 2024 katika Viwanja vya Mwl. Nyerere SabaSaba.

SabaSaba mambo ni moto!

# 48TH DAR ES SALAAM INTERNATIONAL TRADE FAIR 2ND PLACE

Manispaa ya Temeke yaibuka mshindi wa pili maonesho ya kimataifa ya biashara (sabasaba) 2024, katika kundi la manispaa.




www.temekemc.go.tz

# “CLUSTER NI UTARATIBU ULIOANZISHWA NA TAASISI”

Na Sweetbetter Njige
TMC Habari.



Leo Septemba 25, 2024 Manispaa ya Temeke kupitia Wataalam wake wakiongozwa na Mkuu wa Idara ya Biashara Ndg. Ramadhan Gurumukwa na Meneja wa ‘Cluster’ ya Charambe Ndg. Brayson Maleko, imetoa elimu kwa Wafanyabiashara wanaotumia kituo cha kutolea huduma (Cluster) Charambe inayoundwa na kata za Charambe, kilungule, kibondemaji, kiburugwa na Mbagala juu ya masuala mbalimbali ya kibiashara hususani elimu ya kodi, aina za kodi na tozo za halmashauri na vipindi vya kulipa kodi hizo.

Akizungumza katika mkutano huo Mwakilishi wa Mkuu wa Wilaya ambaye pia ni Afisa Tarafa ya Mbagala Bi. Betha Minga amesema

“Kwa kifupi sana ningependa muelewe vituo vya mapato vilivyoanzishwa ni jambo la kitaasisi. Tumeona kwamba tusogeze huduma za mapato kwa jamii baada ya kuona kuna umbali mkubwa wa mtu kutoka Mbande kwenda Manispaa kulipa kodi. Umuhimu wa kulipa kodi tunaufahamu na hata mkigeuka nyuma yenu kuna hospitali inajengwa kwa mabilioni ya fedha, hizo ni nguvu na juhudi zetu wenyewe kupitia hizo hizo kodi”

Aidha Mkuu wa Idara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji Ndg. Ramadhan Gurumukwa amewataka Wafanyabishara kufuata utaratibu uliowekwa ili kufanya biashara zao.

“Kama wewe ni machinga tunafahamu kuna maeneo maalum ya kukaa sio barabarani, kwa walipa kodi tunafahamu kabisa hii biashara yangu hapa ilipofikia nahitaji kuwa na leseni ya biashara”. Alisema Ndg. Gurumukwa

Mkutano huo umehudhuriwa na Waheshimiwa Madiwani, Wakuu wa idara na vitengo kutoka halmashauri ya manispaa ya Temeke na Watumishi wa Manispaa kutoka katika Cluster ya Charambe.



# JWTZ NA JESHI LA UKOMBOZI LA WATU WA CHINA LAGUSA AFYA ZA WANATEMEKE

Na Joanita Joseph,
TMC Habari.




Julai 19, 2024 Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) kwa kushirikiana na Madaktari kutoka Jeshi la Ukombozi la Watu wa China wameendesha zoezi la utoaji huduma bure za uchunguzi wa kiafya na matibabu ikiwemo za kibingwa kwa wakazi wa Temeke ikiwa ni sehemu ya kuadhimisha miaka 60 tangu kuanzishwa kwa JWTZ na miaka 60 ya ushirikiano na Jeshi la China.

Akizungumza katika eneo hilo Daktari Esther John Matoro, Mganga mfawidhi wa kituo cha Afya Mbagala Round table amesema

“Kipekee tunawashukuru sana JWTZ na Jeshi la China, huduma walizozitoa leo ni nzuri na wananchi wamefurahia na wametamani wangekaa zaidi kwakuwa huduma zinahitajika” alisema Dr. Esther

Zoezi hilo limefanyika katika Kituo cha Afya Mbagala Round Table ambapo takribani Wananchi 156 wamepata huduma huku wengine wakishauriwa kuhudhuria kituoni na Bandari gate Namba 02 ambapo huduma zinaendelea kwa msaada zaidi.

Mapema Julai 16, 2024 Meli ya hospitali ya ‘Ark peace’ iliwasili Nchini ikiwa na Madaktari Bingwa pamoja na Vifaa vyote tayari kufanya uchunguzi wa kiafya kwa Watanzania kwa siku 5 kuanzia Julai 17 hadi Julai 22, 2024.

## TEMEKE YAENDELEA KUFANIKIWA UTEKELEZAJI MKATABA WA LISHE

Na Sweetbetter Njige
TMC Habari.

Kaimu mkurugenzi manispaa ya Temeke ACP Andrew Mchome amepokea taarifa za utekelezaji wa afua za mkataba wa lishe kutoka idara na vitengo mbalimbali vya manispaa ya Temeke katika kikao kilichofanyika leo Agosti 15, 2024 ukumbi wa Afya, manispaa ya Temeke.

Akihitimisha kikao hicho kaimu mkurugenzi ACP Mchome amesema kama Manispaa inajivunia kufanya vizuri katika mkataba huo wa lishe lakini jitihada zaidi zinahitajika ili kuendelea kutoa lishe bora hasa kwa wanafunzi mashuleni.

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa lishe Bi. Happy Nkunda amesema manispaa inaendelea kufanikiwa katika utoaji wa elimu ya lishe kwa makundi mbalimbali hasa kundi la wajawazito ili kuhakikisha watoto wanazaliwa na afya njema.

Aidha kupitia idara za elimu msingi na sskondari, manispaa kupitia wataalam wake imeendelea kusimamia upatikanaji wa lishe bora katika saa za masomo kwa kuhakikisha mlo wa mchana unapatikana na kuanzisha kilimo cha mbogamboga katika shule hizo ili zitumiwe na wanafunzi kuboresha lishe na afya.

Kikao hicho cha robo ya mwisho kwa mwaka kimetoa mwanga wa jinsi elimu ya Lishe ilivyoweza kusaidia kuongeza ufaulu kwa wanafunzi kutokana na takwimu zilizotolewa na baadhi ya washiriki wa kikao hicho.

# MIRADI IZINGATIE CHUMBA MAALUM KWA AJILI YA MABINTI

Na Sweetbetter Njige,
TMC Habari.



Leo Agosti 16, 2024 kamati ya fedha manispaa ya Temeke ikiongozwa na mwenyekiti wa kamati hiyo diwani wa kata ya Miburani mheshimiwa Juma Mkenga imefanya ziara ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa ndani ya manispaa.

Akizungumza katika kikao cha majumuisho Mkenga amewapongeza wataalam wa manispaa kwa kazi nzuri ya utekelezaji wa miradi na kumuagiza mhandishi wa manispaa kuzingatia uwepo wa chumba maalum kwa ajili ya wanafunzi wakike. Amesema

"Kunapaswa kuwepo na chumba maalum katika kila ujenzi wa matundu ya vyoo yanayojengwa, tunawathamini sana mabinti zetu wanapaswa kutengewa chumba chao maalum kwa ajili ya matumizi yao muhimu, hilo ni muhimu sana".

Kwa upande wake mkuu wa idara ya Maendeleo ya Jamii Furaha Chiwile amesema kama wataalam wapo tayari kufanyia kazi kwa haraka maelekezo yaliyotolewa na kamati ya fedha ili kuhakikisha miradi inakuwa na ubora na tija pamoja na mahitaji ya wanufaika wa miradi hiyo.

Kamati ya fedha imetembelea miradi mbalimbali ya ujenzi wa shule moya ya sekondari ya ghorofa katika kata ya Mbagala ( shule ya sekondari Mangaya) yenye ghorofa 3, vyumba vya madarasa 16, matundu 40 ya vyoo, miundombinu ya walemavu na ofisi nane inayogharimu shilingi 300,000,000.00 inayotarajiwa kukamilika na kuanza kutumika Januari 2025.

# DC MAPUNDA ATOA WITO KWA NGO'S KUWEKEZA KATIKA MIRADI YA MAENDELEO

Na Shalua Mpanda,
TMC Habari.

**Wito umetolewa kwa mashirikia yasiyo ya kiserikali (NGO's) kuacha kufanya shughuli zao kwa mazoea na hatimaye wawekeze katika miradi ya maendeleo.**




Wito huo umetolewa na Mkuu wa wilaya ya Temeke mheshimiwa Sixtus Mapunda leo Agosti 20,2024 wakati akizungumza na wawakilishi wa Mashirika hayo katika mkutano wa Jukwaa la Mwaka la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali(NaCoNGO) katika ukumbi wa Salvation Army wilayani Temeke.

*Mashirika binafsi ni rafiki mwema wa Serikali na Wananchi*

Mhe.Mapunda amesema ni wakati muafaka sasa kwa Mashirika hayo kufanya mambo yanayoonekana na kuacha kufanya mambo kwa nadharia ili kuweza kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla.

"Kikao hiki kitoke na suluhisho na mjiongeze na kufanya mambo mengine ambayo ni tangible (yanayoonekana) ikiwemo miradi ya maendeleo". Aliongeza Mkuu huyo wa Wilaya

Kikao hicho cha Jukwaa la mwaka la Mashirika yasiyo ya Serikali kwa mwaka huu kimebeba kauli mbiu isemayo "Mashirika yasiyo ya kiserikali ni wadau muhimu washirkishwe kuimarisha Utawala bora".

# TEMEKE YAFANIKIWA UTEKELEZAJI MKATABA WA LISHE

Na Sweetbetter Njige,
TMC Habari.



Kaimu mkurugenzi manispaa ya Temeke ACP Andrew Mchome amepokea taarifa za utekelezaji wa afua za mkataba wa lishe kutoka idara na vitengo mbalimbali vya manispaa ya Temeke katika kikao kilichofanyika leo Agosti 15, 2024 ukumbi wa Afya, manispaa ya Temeke.

Akihitimisha kikao hicho kaimu mkurugenzi ACP Mchome amesema kama Manispaa inajivunia kufanya vizuri katika mkataba huo wa lishe lakini jitihada zaidi zinahitajika ili kuendelea kutoa lishe bora hasa kwa wanafunzi mashuleni.

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa lishe kwa upande wa Idara ya Afya mratibu wa lishe manispaa ya Temeke Bi. Happy Nkunda amesema manispaa inaendelea kufanikiwa katika utoaji wa elimu ya lishe kwa makundi mbalimbali hasa kundi la wajawazito ili kuhakikisha watoto wanazaliwa na afya njema.

Aidha kupitia idara za elimu msingi na sskondari, manispaa kupitia wataalam wake imeendelea kusimamia upatikanaji wa lishe bora katika saa za masomo kwa kuhakikisha mlo wa mchana unapatikana na kuanzisha kilimo cha mbogamboga katika shule hizo ili zitumiwe na wanafunzi kuboresha lishe na afya.

Kikao hicho cha robo ya mwisho kwa mwaka kimetoa mwanga wa jinsi elimu ya Lishe ilivyoweza kusaidia kuongeza ufaulu kwa wanafunzi kutokana na takwimu zilizotolewa na baadhi ya washiriki wa kikao hicho.

# BARAZA LA MADIWANI LAPITISHA MPANGO KABAMBE WA KUONGEZA UWEZO WA UKUSANYAJI MAPATO

Na Shalua Mpanda,
TMC Habari.

Kutokana na ukubwa wa eneo la kijiografia la Manispaa ya Temeke, wingi wa watu na Shughuli zao, Baraza la Madiwani la Manispaa hii leo Agosti 30, 2024 kwa kauli moja limepitisha Mpango wa maboresho ya utoaji wa huduma ya ukusanyaji mapato katika ngazi ya chini ya Manispaa hii ili kuondoa kero kwa Wananchi wanaohudumiwa kwa kusogeza huduma karibu yao ikiwa ni pamoja na kugawanya eneo la halmashauri katika maeneo sita ya kutolea huduma (Clusters).

Akiongoza Mkutano wa Baraza hilo Mstahiki Meya wa Manispaa ya Temeke Mhe.Abdallah Mtinika amesema Manispaa hii yenye idadi ya wakazi wapatao milioni 1 na laki 3 inapaswa kuwa na maeneo mengi ya kutolea huduma ili wananchi wafikiwe kwa urahisi.

Aidha amewataka watendaji walioteuliwa kufanya kazi katika vituo hivyo kufanya kazi kwa weledi na kuweka maslahi ya Taifa mbele.

"Niwasihi ndugu zangu huko mnapoenda kufanya kazi hii mjitume na kuiwezesha Halmashauri kukusanya mapato na kufikisha lengo tulilojiwekea".Alisema Mhe. Mtinika



## LUKUVI ASHUHUDIA MAONESHO BANDA LA MANISPAA YA TEMEKE, SINGIDA

Na Mwandishi Wetu,
TMC Habari.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) Mhe. William Lukuvi ametembelea Banda la Manispaa ya Temeke na Kujionea Bidhaa mbalimbali kutoka kwa Wajasiriamali wanaopatikana Katika Manispaa ya Temeke

Mhe. Lukuvi leo Septemba 10, 2024 amezindua Maonesho ya Saba ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi 2024 yanayolenga kutoa nafasi kwa Wananchi kupata uelewa kuhusu programu mbalimbali za uwezeshaji Wananchi kiuchumi na jinsi wanavyoweza kunufaika nazo.

Halmashauri ya Manispaa ya Temeke kupitia Idara ya Maendeleo ya jamii inashiriki maonesho hayo yanayojiri katika Viwanja vya Bombadia Mkoani Singida.




# MTEMVU: KINABABA WANAPASWA KUSHIRIKI KUNYONYESHA

Na Sweetbetter Njige,
TMC Habari.

Leo Agosti 1, 2024 Halmashauri ya Manispaa ya Temeke imezindua rasmi Wiki ya Unyonyeshaji Maziwa ya Mama Duniani kwa kutoa elimu kwa vitendo katika Zahanati ya Mbande, Chamazi.

Akizungumza katika hafla hiyo Mhe. Mariam Mtemvu Diwani wa Viti maalum na Mwenyekiti wa kamati ya huduma za jamii ambaye pia alikuwa Mgeni rasmi katika hafla hiyo amesema

"Kunyonyesha ni suala la kijamii na kifamilia, Wakinababa mliopo mahali hapa mtusaidie kufikisha ujumbe huko, mama hatoweza kunyonyesha akiwa na mawazo na mahangaiko ya moyo. Tumeelezwa mengi hapa ya kisayansi lakini kwakua mimi ni mama nawakumbusha kunyonyesha kunaongeza upendo baina ya mama na mtoto. Tusidhani hivyo vitu vya dukani ni bora sana kuliko maziwa ya mama tuwanyonyeshe kwa ajili ya afya na ukuaji wao na wakianza kula tuwape vyakula vya asili" alisema Diwani Mtemvu

Kwa upande wake Kaimu Mganga Mkuu wa Wilaya Daktari Philipo Lambo amesema

"Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO) 53% ya Watoto wanapata fursa ya kunyonya baada ya saa moja tangu kuzaliwa na 45% ya watoto wanapata fursa ya kunyonya kwa miezi 6 ya mwanzo bila kuchanganyiwa chakula chochote. Kauli mbiu inatutaka tuzibe pengo la asilimia zilizobaki kwa kuwapa watoto fursa na haki yao ya kunyonya. Tunaendelea kusisitiza watoto wanyonyeshwe katika siku 1000 za maisha ya mtoto kwakuwa kisayansi maziwa asili ya mama yana kinga na ni salama na hayachanganywi na kitu chochote kile tofauti na maziwa mengine"

## TIMU YA WATAALAMU TEMEKE KUJIFUNZA UENDESHAJI KIDIGITALI

Timu ya ukusanyaji wa Mapato ya Halmashauri kupitia vyanzo vyake mbalimbali Manispaa ya Temeke mwezi Agosti, 2024 ilifanya ziara katika Halmashauri ya Manispaa ya Moshi lengo likiwa ni kujifunza zaidi ukusanyaji mapato ambayo ni nyenzo muhimu katika uendeshaji wa halmashauri na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

# ZAHANATI YA KILAKALA YAPANDISHWA HADHI KUWA KITUO CHA AFYA

Na Mwandishi Wetu,
TMC Habari.

**Wananchi wa kata ya Kilakala kupitia Diwani wa Kata hiyo Mheshimiwa Amir Salum (Osama) wamemshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya Afya katika Zahanati ya Kilakala iliyowezesha zahanati hiyo kupandishwa hadhi na kuwa Kituo cha Afya.**



Hayo yamesemwa kufuatia ziara ya mkuu wa mkoa wa Dar es Salaam Mhe. Albert Chalamila wakati akifanya ukaguzi wa miradi ya maendeleo wilaya ya Temeke. Mhe Chalamila amesema.

"Nimpongeze mkuu wa wilaya na mkurugenzi kwa mradi mzuri, marekebisho madogo yapo na nimeelekeza yafanyiwe kazi. Ifahamike, Utejelezaji wa miradi ya afya pamoja na vifaa vyake ni gharama sana. Uwekezaji mkubwa umefanyika hapa. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan anampango wa kuleta bima za afya kwa wote ili Wananchi muhudumiwe vizuri. Tunakatia bima magari, tujikatie bima pia, maisha yana thamani kuliko chombo unachotumia leo. Maelekezo ya mhe. Rais ni sisi viongozi kusimamia vyema sekta ya afya".

Zahanati ya Kilakala imeongezewa mejengo tisa ikiwemo jengo la upasuaji, wodi ya wazazi, jengo la mionzi, walkways, jengo la wagonjwa wa nje (OPD) maabara, nyumba pacha za watumishi, jengo la kufulia, kichomea taka (high taking incinerator) majengo hayo yote yana jumla ya gharama ya shilingi Bilioni 1,009, 334, 356.28 na sasa kimepandishwa hadhi rasmi kuwa kituo cha afya kutoka na ongezeko la miundombinu na huduma zitakazotolewa.

# HALMASHAURI YA MOMBA YAPATA DARASA KUDHIBITI VVU

Na Sweetbetter Njige,
TMC Habari.

Leo Agosti 13, 2024 madiwani wanaounda kamati ya kudhibiti UKIMWI wakiongozwa na naibu mwenyekiti wa halmashauri ya wilaya ya Momba mkoa wa Songwe mheshimiwa Njanvwa Jackson Sihame wamefanya ziara ya mafunzo katika mati hiyo, kaimu mkurugenzi wakili Faraja Nakua na wataalam wa idara ya Afya wakingozwa na mganga mkuu Jonas Lulandala.

Akizungumza katika ziara hiyo mhe. Sihame amesema

"Tumekuja kujifunza namna kamati ya kudhibiti UKIMWI manispaa ya Temeke kuwa nyepesi kwa kushirikiana kikamilifu na wataalam wa ngazi zote na jamii yenyewe"

Aidha madiwani hao wametembelea hospitali ya rufaa ya mkoa wa Temeke (TRRH) na kujionea huduma kwa waathirika wa virusi vya UKIMWI na madawa ya kulevya zinavyotolewa pamoja na mikakati mbalimbali ya elimu na udhibiti inayotolewa na hospitali hiyo chini ya uongozi wa daktari Joseph Kimaro.

Manispaa ya Temeke imeendelea kuwa mwenyeji kwa halmashauri mbalim-




halmashauri ya manispaa ya Temeke na kupokelewa na mwenyeji naibu meya mheshimiwa Anorld Peter, madiwani wanaounda kamke inapanga na kufanikisha udhibiti na kuelimisha zaidi juu ya maambukizi ya UKIMWI. Tumejifunza kuwa, kamati imefanya shughuli bali kwa kushiriki katika mafunzo na kubadilishana utaalam ili kuongeza ufanisi katika kuwahudumia Wananchi.

HALMASHAURI YA MANISPAA YA
**TEMEKE**

# SHIRIKI UCHAGUZI WA SERIKALI ZA MITAA

**TAREHE 27/11/2024**

**KAULI MBIU: "SERIKALI ZA MITAA, SAUTI YA WANANCHI, JITOKEZE KUSHIRIKI UCHAGUZI."**





**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS,**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE**

# TAARIFA KWA UMMA

## MAPOKEZI YA FEDHA SHILINGI MILIONI 613.8 KWA AJILI YA UJENZI WA SHULE MPYA, MADARASA NA MATUNDU YA VYOO.

**Temeke, Dar es salaam, Agosti 30,2024.**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Temeke Ndg. Jomaary Satura anapenda kuutarifu Umma kuwa Manispaa ya Temeke imepokea kiasi cha fedha Shilingi **613,800,000/=** za Kitanzania kutoka Serikali kuu.

Fedha hizo zimeelekezwa kutekeleza Miradi ya maendeleo kwa Idara ya elimu msingi ambapo itatekeleza ujenzi wa shule mbili (02) mpya za msingi, ujenzi wa madarasa mawili (02) na matundu sita (06) ya vyoo kwa elimu ya awali.

Aidha kiasi hicho kinajumuisha fedha za ufuatiliaji, ujenzi pamoja na usimamizi kwa ngazi ya shule.

Mapokezi ya kiasi hicho cha fedha yanaendelea kudhihirisha jitihada za Serikali ya Awamu ya Sita katika kuboresha miundombinu na kurahisisha upatikanaji wa elimu kwa watoto wa Kitanzania kuanzia ngazi ya awali.

Uongozi wa Manispaa ya Temeke unapenda kumshukuru Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutoa fedha hizo kuboresha Sekta ya elimu na mazingira ya upatikanaji wa elimu kwa wazazi na wanafunzi, na kuahidi kuendelea kushiriki kikamilifu katika usimamizi na utekelezaji wa miradi ya maendeleo kama inavyodhamiriwa, kwa maendeleo endelevu.

JOANITA JOSEPH
KAIMU MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI
**HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE**

JARIDA HILI HUTOLEWA NA
KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI
HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE
S.L.P 46343 TEMEKE, DSM.
SIMU: +255 22-2928132
NUKUSHI: +255 22-2928137
BARUA PEPE: TEMEKE@TEMEKEMC.GO.TZ